



REPUBLIC OF KENYA
COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI
THIRD ASSEMBLY-THIRD SESSION

THE HANSARD

Tuesday, 7th May 2024

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 9:30 a.m.*

[The Deputy Speaker (Hon. Kombo) in the Chair]

PRAYER

PAPERS LAID

THE KILIFI COUNTY PROGRAMME-BASED BUDGET ESTIMATES FOR THE FINANCIAL
YEAR ENDING 30TH JUNE 2025

Hon. Emmanuel: Hon. Speaker, thank you so much for this opportunity. Today being 7th May 2024, I beg to lay the following Paper on the Table: -

The Kilifi County Programme-Based Budget Estimates for the Financial Year ending 30th June 2025.

Thank you.

(Hon. Emmanuel laid the document on the Table)

THE 1ST, 2ND AND 3RD QUARTER REPORTS FOR THE DEPARTMENT OF GENDER, CULTURE, SOCIAL SERVICES, SPORTS, YOUTH AFFAIRS, SPECIAL PROGRAMMES AND DISASTER MANAGEMENT

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Emmanuel: I also beg to lay the following Papers on the Table: -

The First, Second and Third Quarter Reports for the Department of Gender, Culture, Social Services, Sports, Youth Affairs, Special Programmes and Disaster Management.

Thank you.

(Hon. Emmanuel laid the documents on the Table)

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Hon. Members, the Kilifi County Programme-Based Budget Estimates for the Financial Year ending 30th June 2025 has been committed to the Budget and Appropriations Committee and all the Sectoral Committees of this esteemed House.

The Second Paper, which is the First, Second and Third Quarter Reports for the Department of Gender, Culture, Social Services, Sports, Youth Affairs, Special Programmes and Disaster Management, has been committed to the Committee on Gender.

REPORT OF THE HEALTH SERVICES COMMITTEE ON THE STATUS OF SUB-COUNTY
HOSPITALS IN KILIFI COUNTY

Hon. Ziro: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for giving me this opportunity. I beg to lay the following Paper on the Table: -

Report of the Health Service Committee on the status of Sub-County Hospitals in Kilifi County.

Thank you.

(Hon. Ziro laid the document on the Table)

NOTICE OF MOTION

ADOPTION OF THE REPORT OF THE HEALTH SERVICES COMMITTEE ON THE STATUS OF SUB-
COUNTY HOSPITALS IN KILIFI COUNTY

Hon. Ziro: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I beg to give a Notice of Motion: -

THAT, this House adopts the Report of the Health Services Committee on the status of Sub-County Hospitals in Kilifi County laid on the Table of this House on Tuesday, 7th May 2024.

Thank you.

MOTION

HARDSHIP ALLOWANCES FOR ECDE TEACHERS IN KILIFI COUNTY

Hon. Mohamed: Thank you, Mr. Speaker. I beg to move the following Motion: -

THAT, aware that a good number of ECDE (Early Childhood Development and Education) Teachers in the County are exposed to hazards and difficulty because of the nature and location of their work.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

FURTHER AWARE THAT, for many years, ECDE Teachers have been working in very remote areas with no water and electricity, areas with high poverty incidences and occasions, and violent attacks yet no allowance has ever been provided.

COGNIZANT TO THE FACT THAT, the above category qualifies for hardship allowances as described by UNICEF (United Nations Children's Fund) and the Kenya Public Service.

ALIVE TO THE FACT THAT, efforts by the National Government to allocate ECDE teachers hardship allowances through the Teachers Service Commission (TSC) have not materialized and teachers continue to work in hostile and high-risk environments.

NOW THEREFORE, this House wishes to resolve that the County Executive Committee Member in charge of Education undertake a mapping exercise of Teachers that ought to benefit from these allowances, budget for it and have it reflected in their salaries in the soonest time possible.

Mr. Speaker, I wish to submit that this is a Motion which brings us to at least look at the conditions our ECDE Teachers are working in. In this Country, the Teachers who are under TSC are provided with hardship allowances wherever they are working in hardship areas. I will give an example of Bamba Ward; this is one of the hardship areas where most of us can agree that the working conditions in Bamba are not that conducive and the Teachers under TSC who work in the same environment, same institutions as our teachers in the ECDE are provided with hardship allowances.

It is for this reason that I wish to beg this House to approve this Motion so that our ECDE teachers who are mostly our sisters, daughters and brothers at least enjoy the hardship allowances so that they can also feel they are part and parcel of the teaching fraternity of whom I can say they are doing much more work than the primary teachers.

We take our ECDE children to school and as we know as parents it is very difficult to teach a small kid. These people are handling the little kids in a very difficult environment. I can give an example of an ECDE Teacher who is working in Chamamba in Goshi Sub-location, a place where there is no transport and there is no house where the teacher can sleep. The teacher has to reside in Bamba Town, and the nearest point can be Jila or Shirango where he or she has to use a motor bike, and it can cost him Kshs500 a day. That is the place she or he goes to work.

There is no water at the same place where she/he goes to work and there is no water and toilet. Imagine someone working in such an environment teaching our children and at the end of the month, someone with the same environment in the same institution enjoys a hardship allowance over and above the salary that the TSC is paying. It is demoralizing and today I wish that this House considers and approves this Motion so that our brothers and sisters can also enjoy the hardship allowances over and above their salaries. With those few remarks, I wish to request hon. Zia to second the Motion.

(Hon. Zia seconded)

(Question proposed)

AMENDMENTS TO MOTION

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Mumba: Thank you, for this opportunity. I want to move an amendment to the Motion of Hon. Mohamed on hardship allowances for ECDE teachers.

Notice is hereby given that Hon. Mumba intends to move the following amendments to the Motion on hardship allowances for ECDE teachers during this plenary:

THAT, the title of the Motion to be amended by inserting the words “VTCs Instructors” after the word “ECDE teachers”.

Two, that the same words be inserted in the first and third lines after the word “ECDE teachers”.

Three, insert the phrase “Instructors both in ECDE Centres and VTCs (Vocational Training Centres)” in the second last sentence of the prayer immediately after the word “Teachers”.

Before I ask hon. Changawa to second, I wish to make a few remarks. I want to commend hon. Mohamed for the move to make sure that our ECDE teachers are given an environment whereby they can compete with the other teachers so that they may not see them as lesser beings as they operate under the same environment. It is indeed my wish that we consider those instructors in the VTCs across the county because they are also undergoing the same conditions.

In this regard, that is what informed me to make sure that we move this amendment so that we address the issue of the teachers because they do the same job under the same harsh conditions.

If you allow me, I will move briefly to the objects of the 2010 Constitution which we are all housed in and guided by in this country, in Article 174 on (e), (f), and (g) just to fortify the information on why we are pushing for the ECDEs teachers and instructors of the VTCs to be considered in the hardship allowances. If you go to (e), it says: “To protect and promote the interest and rights of minorities and marginalized communities.”

The other day I had the opportunity to attend a meeting at a place called Bombi in Adu by the name Habura. Indeed, Mr. Speaker, those communities are marginalized. There are institutions there and the same people require the same services. The conditions are not favourable, most of the payment is consumed by the daily expenses of transport and other expenses. These teachers do not have a good environment to work in. (f) says; “to promote social and economic development and the provision of proximate, easily accessible services throughout Kenya.” As it is now, it is not easily accessible because the teachers themselves find it very hard to access these institutions. So again, we are behind the 2010 Constitution, and I believe this Motion is timely at least now we are realizing the objects of this Constitution that we embraced in 2010.

When you go to (g) it says: “to ensure equitable sharing of national and local resources throughout Kenya”. If these teachers spend all their salaries on daily expenses, indeed there is no equity in resource allocation. We expect everyone at the end of the day the salary you are getting to propel you into doing other things in terms of your personal development not just to make you run daily expenses as you execute your roles in the government. I believe this Motion is timely and if you have a heart for these people and our people, indeed some of them, as he has said are our sisters, brothers and mothers above all they are our voters. I am reminded some are our wives, so it is very important we consider this matter so that when they are laughing at home you can enjoy good services for those who have wives who are working in these environments.

If they have a hard time in the day at work, it will be unfortunate that at home they will also have it rough, and we also want more children to be born so that more votes can be registered in these counties. As much as we want to move for the higher seats, we must make

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

sure that we bear more kids to increase the votes. These are the ways of improving the environment, even in our homes, making sure they are happy for us now to bear more children. I urge Members we approve this amendment so that it can now go to the mother Motion and approve it as well with amendments. With those many remarks, I call upon hon. Changawa to second. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Thank you, hon. Chengo (Mumba) for the detailed submission of the amendments.

(Hon. Changawa seconded)

(Question of the amendment proposed)

Hon. Kubo: Asante sana, mheshimiwa Spika. Naunga mkono Hoja hii ikiwa na mabadiliko kwa sababu sisi kama Wawakilishi wa watu wa Kilifi, tunajaribu sana kuhakikisha kwamba elimu katika Kilifi inakuwa ya hali ya juu na ndio elimu iweze kuwa katika hali inayostahili lazima pia tupatie motisha walimu ambao wanafundisda hawa watoto. Mimi pia ni mmoja wa Wanakamati wa Elimu na ni mmoja wa wale ambao napenda watu wangu wa Kilifi. Naunga mkono Hoja hii. Asante sana, mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Waheshimiwa, pengine niwakumbushe kwamba wakati huu tunaongea kuhusu haya mabadiliko ambayo yameletwa na mheshimiwa Thomas Chengo (Mumba). Kwa hivyo, ni mpaka tukubaliane na haya mabadiliko halafu tutarudi kwa ule mjadala wa hapo awali.

Hon. Ngirani: Thank you, Mr. Speaker. I rise in support of the amendments that have been brought before this House by hon. Thomas Chengo (Mumba). I support the amendments because I believe VTC instructors and ECDE teachers are of the same calibre as they are both under the same department; they are in all corners of the county, and all undergo the same treatment of hardship. It is good enough to have both receiving the hardship allowances. Thank you, Mr. Speaker.

Hon. (Ms.) Mariam: Asante sana, mheshimiwa Spika. Naunga mkono mabadiliko ambayo yameletwa na mheshimiwa Thomas Chengo (Mumba) na sababu ni kuwa tukisema kuwa walimu wa ECDE wako katika mazingira ambayo si mazuri tukiangalia pia zile VTC zetu kule ziko sehemu moja na hizo ECDEs kwa hivyo, kuwapatia motisha lazima tuwapatie wote. Asante.

Hon. Changawa: Thank you, hon. Speaker. I stand to support the amendment in that we want to kill two birds with one stone, and we do not want a scenario whereby after a few days we get a Motion for capitation of VTCs. I support the amendment. Thank you.

Hon. Brown: Asante, Bw. Spika. Nasimama tu kwa hiyo Hoja ya kuunga mkono mabadiliko haya ya kuwa kitengo cha walimu wa wale wanafunzi wa chekechea na wale wengine waitwe wakufunzi kwa upande wa mafundisho ya vyuo. Asante, Bw. Spika.

Hon. Shehe: Thank you, Mr. Speaker. Let me congratulate hon. Mwambire (Mohamed) and the Minority Leader for such a consideration on the alteration and proposals of this House to support those amendments through our CECMs. I think our teachers have been having hell in the areas they come from. I do not know whether the TSC (Teachers Service Commission) know where they post the teachers that even without the students from the ECDEs, the VTCs are also getting similar situations whereby others are celebrating on the other hand and others are really in a bad mood; even the type of working relationship has been deteriorating because there is an

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

open separation of reactions when it comes to the end of the month. I wish our honourable House to take this one very candidly and give it a good nod that both the VTCs and ECDE teachers get this consideration as early as possible so that at least they can be motivated in their educational root where they are following giving our students the services that are expected from the teachers. Thank you very much, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Hon. Thaura.

Hon. Thaura: Thank you, Mr. Speaker. I think by the mood of the House, the issue about the amendment is already resolved. So, Mr. Speaker, my prayer is we go back to the main agenda. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Are you sure? I asked whether, you are sure.

Hon. Thaura: Yes, I am sure.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Okay, thank you. So, hon. Thomas Chengo (Mumba) we give you a chance to reply before we put the Question.

Hon. Mumba: Thank you, Mr. Speaker. Mine is just to thank the House for unanimously accepting the amendments and it is a good gesture. That is a clear indication that Motion will find the light of the day. So, thank you, Mr. Speaker.

(Question, that the words to be added be added, put and agreed to)

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): So, hon. Members, allow me to propose the amended Motion.

(Question of the Motion as amended proposed)

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): So, this Motion is now ready for debate.

Hon. Brown: Asante sana, Bw. Spika, kwa fursa hii tena ambayo umenipatia kwa ajili ya hii Hoja ambayo iko katika Bunge letu tukufu la Kilifi.

Kwanza, wacha nimpongeze mheshimiwa Mohamed Mwambire kwa kuleta maono haya ya kuzidi kupanua uchumi na kuzidi kupanua hazina zetu za nyumbani na pia kusaidia katika kutoa umaskini watu wale wote ambao ni watendaji kazi katika Kaunti yetu. Pia, ninaenda kuzungumza mjadala ambao umeletwa na mabadiliko na mheshimiwa wetu Thomas Chengo (Mumba).

Niko na maswala matatu ambayo ningependa kuchangia kwa ajili ya mjadala huu. Mheshimiwa Spika, ni jambo la manufaa ikiwa Bunge litakuwa lina uwezo wa kukaa na kuona ni mahali gani kuna ukosefu ama kuna dhuluma ama kuna haja ya kuzidi kuinuliwa. Kusema ukweli, mimi nikiwa mwalimu, walimu hawa ambao ni walimu wa chekechea na pia walimu wale ambao wanafanya kazi ama wanafundisha katika vile vyuo kwa sababu katika tafsiri nimeangalia *instructors* ni walimu na wale ECDE pia ni walimu kwa hivyo katika lugha sanifu ya Kiswahili *instructors* na *teachers* wote ni walimu.

Kwa hivyo, kuna hali zilikuwa kama zinaonekana dhuluma za utendaji kazi kwa wale walimu ambao wanafanya kazi ngumu sana. Watoto wanatoka majumbani wakiwa wako na lugha ya mama lakini wanasaidiwa kwa hali ngumu mpaka mtoto ajifahamu kwamba yeye pia ni mwanafunzi na awe na uwezo wa kujua kwamba mimi nina maono pia katika maisha ya kutafuta njia hii na ile.

La pili ni kwamba, serikali inaangazia sana walimu ambao wameenda katika vyuo wanaonekana kwamba wanachukua katika yale marupurupu yao katika sehemu ziko na kazi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ngumu pia wakati mwengine pia kuna ukame kama vile ulivyopata kusikia wenzangu waliotangulia kwamba hata mwalimu anachukua pesa zake zote anazimalizia kwa Barabara; hana uwezo wa kujiendeleza.

Hili ni jambo la maana sana katika mjadala huu ikiwa utapitishwa. Watapata kuwa na uwezo wa kujikimu kimaisha ili kujiendeleza kimaisha kwa hivyo mimi kwa dhati naunga mkono nikiamini kwamba Bunge hii kila mmoja anasikia furaha na pia walimu wote katika Kilifi *County* mimi nawaunga mkono kwa dhati kwamba tuzidi kushirikiana kwa ajili tupitishhe Hoja hii. Asante sana, Bw. Spika.

Hon. Zia: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ili kuleta changizo zangu. Wacha tushukuru kwa mjadala ambao uliweza kuletwa hapa na mheshimiwa Mwambire kutoka kule Bamba na yale marekebisho ambayo yameweza kufanywa na mheshimiwa wa Tezo mheshiwa Tom Chengo Mumba.

Haya yote ni kwa ajili ya ufanisi mzuri kwa wafanyikazi wetu hasa upande ule wa ECDE na upande ule wa vyuo vya ufundi. Kwa kweli ni kwamba hawa *instructors* na hawa *ECDE care givers* wanapitia mambo makubwa sana. Ukikumbuka ya kwamba ulipokuwa mtoto mdogo yule ndiye mtu wa kwanza kabisa yule *care giver* pale chini ambaye anakulea kwa sababu mzazi anakuleta shule katika kile kiwango cha chini kabisa. Nimeileta hiyo picha kwa sababu tunaona kwamba pengine hata mtu anajikojolea kojolea mtoto mdogo lakini *care giver* ni yule mwalimu ndiye ambaye anashughulika kwa kila kitu.

Kuna wale ambao wako huku *town* na wale ambao wako katika sehemu zile za mbali hasa kule Adu *Ward* ama kule Bamba ama kule Dingiria. Ni sehemu ambazo ni za ukame hata walimu wanapishana pishana na ndovu ambao wanasumbua sana katika zile sehemu. Lakini unamwona yule mwalimu anatembea katika huo msitu kuhakikisha kwamba mtoto yule ambaye ni wa hapa Kilifi anapata elimu. Ni hali ngumu kiasi ya kwamba anahitaji pia na yeye malezi. Ukiangalia ule mshahara ambao anapata mwalimu anapata kama shilingi elfu kumi na saba (17,000), halafu anakatwa hizo pesa; mwisho wa siku yeye pia ana mkopo na mwisho wa siku ana pata kama shilingi elfu mbili ama elfu tatu (2,000/3,000) ambazo sasa anaenda nazo nyumbani kwa mwezi. Hapo hapo kuna kulipa nyumba; kuna mahali hapo anategemewa. Ukiangalia hivi ni kwamba hawa watu wanapata shida sana. Mimi nimesimama hapa nikisema ya kwamba acha huu mjadala upite ili waweze kufaidika hawa watu wetu.

Tukumbuke ya kwamba, mheshimiwa Spika, kunao hata pia wafanyikazi lakini hiyo itakuja baadaye; wale wafanyikazi ambao wako upande wa hospitali ambao saa hii hawajapata marupurupu yao. Nimekuambia kwamba hiyo tutaileta hapa.

(Hon. Grace stood on a Point of Order)

Hon. (Ms.) Grace: Asante, Bw. Spika. Sheria ya Bunge inasema mheshimiwa aliye kwa Sakafu anafaa kutumia lugha moja mpaka mwisho. Ninaomba mheshimiwa aliye kwa Sakafu kama ameamua kuongea Kiswahili sanifu aongee Kiswahili sanifu kutoka mwanzo mpaka mwisho. Asante.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante kwa hayo marekebisho. Nafikiri mheshimiwa Samson (Zia) hiyo iko wazi. Tumia lugha moja ambayo utaichagua mwenyewe. Endelea.

Hon. Zia: Wale walimu wa vyuo vya ufundi na walimu wa chekechea... kwa hivyo ni kwamba mimi ninaunga mkono yale marekebisho ambayo yameweza kufanywa na tuweze kupitisha hii Hoja ambayo imeweza kuletwa kwa hili Bunge. Asante sana.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Mheshimiwa Zia, nataka nikupongeze kwa sababu tulipoweka lile swali wewe peke yako ndiye umekataa mabadilisho lakini nakushukuru kwa kuwa umebadilisha mawazo na ukachangia kuunga mkono hii Hoja.

Hon. (Ms.) Sidi: Thank you, Mr. Speaker. I rise to support the Motion with maybe a few reservations. I do not know if the County one; will be able to take up the wage bill that will come with this Motion.

Two; maybe in some of the recommendations we can start recommending that ECDE teachers should come from the same ward so that we check our costs and the money that we get. So, if the ECD is in Kayafungo let the teacher also come from Kayafungo. This will also help to elevate our people in our wards to ensure that they are the ones who are also teaching our children.

Third and maybe last, maybe also we should then check one in their pay slip, is that allowance there now or not? This is because I feel that maybe some have, but anyway, most of them are not employed by the county and they are being paid by the parents in the ECDEs. So, I do not know if those will not be affected by this or if they would be asking for more money from the parents to add so that they can be in the same pay grade as the ones that are employed by the county. I rise to support this Motion. Thank you.

Hon. Juma: Asante, Bw. Spika kwa kunipa nafasi na mimi niweze kusisitiza jambo mahali fulani. Kwanza kabisa, naunga mkono wote na mheshimiwa wa Bamba kuweza kuleta maswala haya na vile vile, mheshimiwa Thomas Chengo Mumba kwa kuweza kuongezea na kuweza kuelekeza mambo haya moja kwa moja kulingana na mujibu wa Sheria ya Katiba yetu ya Kenya.

Hii itakuwa imewapa motisha wale wafanyikazi wa Kaunti hii yetu tukufu ya Kilifi na kusisitiza zaidi kulingana na sheria hizo ambazo zimezungumziwa. Vifungu kadha wa kadha vimeonyesha kuwa Kilifi Kaunti basi ni moja wao ya zile Kaunti ambazo zimetengwa na mambo kama yale kwa mujibu wa sheria.

Naomba kusisitiza kwamba hata zile senti za usawa na nikinukuu “*Equalization Fund*” pia ziletwe katika wadi zote thelathini na tano (35) wala si Wadi kadhaa ikizingatiwa kuwa *Kilifi County* inapata mgao mkubwa Kenya nzima. Ni baadhi ya zile *County* ambazo zinapata mgao mkubwa. Sioni haja ya wadi kadhaa ziwe zinapata fedha za usawa na wadi nyengine ziwachwe. Tukizingatia kwamba walimu wote wa chekechea wa Kilifi Kaunti waweze kunufaika. Zile fedha nazo za *Equalization Fund* pia zigawanywe kwa wadi zote wala zisiende kwa wadi kadhaa peke yake. Asante, Bw. Spika kwa kunipatia fursa hii.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante, Mheshimiwa Juma Chengo, kwa changizo zako. Mheshimiwa Elina Mapenzi wakati ni wako.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi ili mimi nami nichangie Hoja hii ambayo inajadiliwa katika Bunge hili la heshima. Vile vile, nipongeze maana utaratibu wa Bunge leo unatembea vizuri na taratibu zinafatwa vizuri. Pia, nampongeza mheshimiwa Mohamed Mwambire kwa kuleta Hoja hii ambayo moja kwa moja inamgusa yule mwana Kilifi. Ninatia msisitizo kwa wale wote ambao ni waheshimiwa ndani ya Bunge hili waweze kuleta mada kama hizi ambazo moja kwa moja zinamgusa mtu wa Kilifi na zinapoletwa basi tuzipitishie mara moja.

Tunapojadili hii Hoja tusingalie swala la fedha. Hapa Kilifi kwetu tuna pesa za kutosha na serikali kuu pia inatupatia fedha za kutosha. Inawezekana swala hili lisiangaliwe leo wala kesho lakini likawekwa katika mipangilio ili mbeleni liwe linaweza fanyiwa kazi. Kwa hivyo, tusingalie changamoto za kifedha saa hii maanake tunaendeleo kuikuza Kilifi. Tunakusanya

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ushuru kutoka sekta mbalimbali na natumaini tutafikia mahali Kilifi nasi tuweze kujibeba vizuri. Kwa hivyo, swala la kifedha tuliweke kando tuangalie hii Hoja maana ni jambo la muhimu sana kwa mfanyi kazi yeyote si tu wa ECDE bali mfanyi kazi yeyote anastahili kupewa hii posho ya shida ikiwa yuko kwenye mazingira ya shida maana ni hii posho ndio itamuwezesha yeye utendaji kazi wake utakuwa vizuri kwa ile sehemu yake ya kazi.

Tunahitaji kuwapatia motisha hawa walimu maanake kuna changamoto nyingi wanakutana nazo. Changamoto za Kilifi tunazijua ikiwa barabara. Wadi nyingi hapa Kilifi zinakumbwa na changamoto za barabara. Ukiangalia kama Wadi ya Ganze, Bamba, Jaribuni, Adu na Marafa, yale ni maeneo ya shida hususan ukiangalia barabara za kule.

Hata katika mahali kwa malazi kwa wale walimu, unakuta katika maeneo ya shule hakuna nyumba nzuri ambazo walimu wale wanaweza jihifadhi ili kesho yake waamke na waweze kuenda kupeana huduma kwa wale watoto. Kwa hivyo, inawalazimu kusafiri. Barabara zikiwa mbaya usafiri wa haraka ni boda boda na boda boda nao wanaongeza gharama kulingana na hali za barabara. Kama hawatapata haya malipo, uwezekano wa hawa walimu kufika maeneo ya kazi kuchelewa upo na wanapofika kuchelewa basi watoto wetu ndo huumia. Kuna changamoto hasa ya mabadiliko ya anga; wakati anga inabadilika hasa wakati wa mvua, maeneo yale ya shida yanakuwa vigumu kupita.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): There is an intervention from Hon. Zia.

Hon. Zia: Asante Mheshimiwa...

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Ungetaka kuongea kuhusu nini?

Hon. Zia: Nimesimama kwa hoja ya nidhamu lakini atufahamishe sisi huyo mheshimiwa ambaye yuko sakafuni.

(Laughter)

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Endelea, nidhamu gani ama kitengo gani cha nidhamu?

Hon. Zia: Ya kwamba nataka atwambie kwa mfano kama Malindi kuna barabara imeharibika, je huyo mwalimu anaweza kupewa *hardship allowance* ama iko vipi maana nakosa kumuelewa chenye anakiongea.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Sasa mheshimiwa Zia, hilo si swala la nidhamu? Tafadhali kaa chini mheshimiwa Elina Mapenzi aendelee.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Asante, lakini pia ni vyema mheshimiwa Zia aweze kufahamu maana tunaongozwa na sheria ambazo pia tunaangalia serikali kuu inafanya nini katika swala hili.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Kuna *intervention* nyengine mheshimiwa Elina Mapenzi kutoka kwa mheshimiwa Grace Wambui.

Hon. Grace: Asante, Bw. Spika. Samahani mheshimiwa Elina Mapenzi, nimesimama hapa maana nimegadhabishwa na mheshimiwa aliyetoka hapa kumpinga mheshimiwa Elina Mapenzi. Heshima ni amuite mheshimiwa si huyu. Kwa hivyo naomba asimame amuombe mheshimiwa Mapenzi msamaha. Hapa hakuna 'huyu' ni dharau na mimi kama mwanamke katika hili Bunge ningepomba mheshimiwa Zia asimame amuombe msamaha mheshimiwa Elina Mapenzi.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Mheshimiwa Grace Wambui, asante kwa hiyo *observation*. Mheshimiwa Samson Zia umepewa nafasi ya kuomba msamaha.

Hon. Zia: Mheshimiwa Nisamehe.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Laughter)

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante. Kaa chini mheshimiwa. Endelea Mheshimiwa Elina Mapenzi.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Ni sawa sawa mheshimiwa Zia. Vile vile, nataka nikufahamisha kwamba serikali kuu ina mipangilio yake ambayo inafuatiliwa kulingana na ajira, mishahara na marupurupu ya wafanyi kazi. Kwa sababu tunaishi sehemu tofauti tofauti, utakuta Malindi *Town* kwa mfano hiyo ni *Ward*, hapa barabara huwezi zilinganisha na Adu ama Magarini lazima utofauti utakuweko. Kwa sababu hiyo basi, naona hapa Kilifi tuige yale yanafanywa na Serikali kuu kulingana na mishahara na marupurupu ya wafanyi kazi. Kwa hivyo, hapo nimezungumzia kuhusu swala la barabara ambayo ni changamoto kwa maeneo yale ya shida ambapo posho la shida lazima hawa walimu wapewe.

Vile vile, nilikuwa nazungumzia kuhusu mabadiliko ya hali ya anga nikasema mara nyingi inabadilika. Hakuna aliyetarajia kwamba tulikuwa tutakumbwa na mafuriko. Mimi mwenyewe jana nilikuwa naja Bungeni, kufika pale Jilore huku upande huu ni mto upande huu mwengine ni ziwa. Maji yamevuja mpaka yanamiminika kwa ziwa na barabara imefunikwa. Sasa maeneo kama yale ni yale tunazungumzia kuhusu *hardship*. Mimi ilinilazimu nirudi tena mpaka maeneo yanaitwa *Pishi Mwenga* nizunguke tena hadi *Sosobora* nishike sasa msitu wa Sosobora mpaka nifike *Chain barrier* umbali ambao ni kama nimetoka Jilore hadi Malindi na nirudi tena Jilore.

Nikizungumzia hivyo, nazungumzia vitu ambavyo naviona maana naishi katika maeneo yale. Mwalimu yule anapopewa yale marupurupu ndio huo uwezo wa kuchukua hizo fedha abadilishe njia afike yale maeneo ya kazi. Uwezo usipokuwepo itakuwa kama mimi nilivyoweza kurudi kwa nyumba na kulala maana sikuwa na mafuta ya kunipeleka kule na kurudi huku. Ninasema walimu waweze kuangaliwa katika mipangilio ya hii Kaunti na waweze kutengewa hizi fedha ziweze kuwasaidia.

Vile vile, wanapopatiwa hizi fedha, kila mfanyikazi, Mkenya ama mwana Kilifi, tunaishi majira ambayo ni ya utandawazi. Mawasiliano yamerahisishwa; unaweza kusoma kupitia mitandao kwa Kiingereza tunaita *internet*, Kiswahili tunaita mtandao. Kila mtu angefurahia kuishi katika mazingira hayo lakini tunakuta hawa wafanyi kazi wetu ama maeneo yale, wale wafanyikazi ama wale wanaishi kule hawawezi kufikia huduma zile na ni changamoto. Kwa hivyo, wanapopewa hii mishahara wana uwezo wa kununua vile vidubwasha kwa Kiingereza nitanukuu vinaitwa *WiFi gadgets*. Wanaweza kununua na pia wao wakawa na wengine katika ulimwengu huu wa kisasa na wakasaidika katika kutafuta habari kuhusisana na maswala ya elimu na wasaidie watoto katika sehemu hiyo.

Kwa hivyo, naunga mkono hii Hoja na tuiptishe na pia *Executive* waweke mipangilio ya hawa walimu waweze kupata haya marupurupu. Asante sana mheshimiwa Spika.

Hon. Ngirani: Thank you, Mr. Speaker. First and foremost, let me take this opportunity to thank the original Mover of this Motion hon. Mohamed and the Mover of amendment hon. Mumba.

Mr. Speaker, where I come from, we say when you inherit a deceased wife; you inherit with the children plus everything. The deceased has left, Mr. Speaker, we as the County Government under the Fourth Schedule inherited a lot from the National Government, one being the function of education, but we only inherited the devolved function of the ECDE and the

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

VTCs. The primary school teachers normally receive hardship allowances so I guess we should have inherited hardship allowances for the ECDE and VTC teachers.

Mr. Speaker, I will give an example of an ECDE in my ward by the name of Mapotea. Mapotea is at the further end of Ganze Ward bordering Tsavo National Park where there is always an invasion of wild animals like elephants, hyenas, etc. I remember the County Government deploying an ECDE teacher at Mapotea. That teacher only survived a month, and she could not survive the hardship of that area because even to get to a shop you must trek several kilometres and so there is a need for such hardship allowances for such remote schools. There will be that elevation of financial stress caused by unexpected events such as the invasions of such animals. There is a story I shared with one of our ECDE teachers in those remote areas, whereby even the students normally come to school hungry. Even the snack or fruit that the teacher has carried forces him or her to share with the kids and they do not have a lot. They wish they could have a lot, maybe they could buy more snacks for these students.

Mr. Speaker, they also trek because the motorcycle charges are normally very high. Why, because of the poor infrastructure of the roads and generally the hardship life these motorcycle raiders undergo. So, Mr. Speaker, the ECDE teachers, and VTC instructors in such areas undergo trauma and stress due to the hardship environment that they face in those areas. Therefore, it is on a high note that this Motion is going to elevate some stress and traumas that these ECDE teachers and VTC instructors undergo. There being no difference between primary teachers and ECDE teachers, I support this Motion that ECDE teachers just like their counterparts in Primary and Secondary Schools receive these hardship allowances. With those few remarks, I stand in support of this Motion. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Hon. Tete.

Hon. Tete: Asante, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi hii ili niungane na wenzangu katika Hoja hii ya kuboresha elimu na uchumi kwa walimu wetu wa chekechea na vyuo vya ufundi. Kwanza, nichukue nafasi hii kupongeza waheshimiwa walioleta Hoja hii ya kutetea walimu wa chekechea katika eneo letu la Gatuzi la Kilifi na vile vile aliyetuletea mabadiliko ya kuboresha Hoja hiyo ili watu wetu katika jamii wasaidike.

Tuko katika nyakati za ugatuzi na napenda kushukuru kwanza mheshimiwa Raila Amollo Odinga aliyepigia upatu mkubwa sana kufikisha ugatuzi mashinani. Lengo kuu lilikuwa ni wananchi wote katika Taifa hili la Kenya kusaidika mbali na Serikali Kuu ilipokuwa imebeba kila kitu, huku wananchi wakilalamika fedha zije mashinani na zitekeleze malengo ili kuona kila mlengwa anasaidika.

Mheshimiwa Spika, kila kazi ni kazi lakini zengine tunazikimbilia kwa sababu zile zinastahili kufanywa zimeisha na mahali ambapo tumefika tunaona walimu ile nafasi yao imekimbiliwa sana si kwamba inapendeza, lakini ndio kazi ambayo asiyekuwa na namna anaenda kuisomea ili aseme angalau hii ina wepesi wa kupatikana asiangalie hata mapato ambayo yako pale. Mimi ninaomba kazi ya walimu itambulike kama kazi na ipewe heshima na kila mmoja awe anaweza kuikimbilia kama kazi sawa sawa na udaktari. Ningeomba kazi ya uwalimu iweze kutambulika kama...

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): There is an intervention from hon. (Ms.) Mapenzi.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Samahani sana...mheshimiwa aliye kwa Sakafu amesema kwamba watu wanakimbilia kuwa waalimu si kwamba wanataka kufanya ile kazi, ni kwa kuwa hakuna namna. Nataka aombe msamaha. Kutoka moyoni, mimi nilisomea uwalimu na sio kwamba nilikuwa sina namna na hilo neno litarudisha nyuma motisha ya watu kule nje wanaoazimia kuwa walimu. Nataka aombe msamaha sisi na wana Kilifi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Mheshimiwa Tete, ombi la mheshimiwa Elina lina uzito wa kutosha kwamba uombe msamaha kwa hilo tamko.

Hon. Tete: Mimi huwa mwepesi wa kuomba msamaha na hilo sio zito kwangu ila naomba achukue kauli yangu na kuunganisha ataona kwa nini nimesema hivyo.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Kulingana na vile alivyonakili, matamshi yako hayakuwa mazuri ni muhimu utoe hayo maneno.

Hon. Tete: Nachukua nafasi hii kuomba msamaha kwa maneno niliyosema, lakini kwa hatua niliyopiga itasaidia mwengine kuelewa ni nini kilichokuwa kinaendelea.

Bw. Spika, ninaendeleza kuunga mkono Hoja hii kwamba mwalimu kwa wanafunzi ama wazazi ni mtu wa maana sana. Nakumbuka kuona maandamano ya walimu, wao wenyewe wakisema kwamba wamedharauliwa wanataka haki zao. Hawaoni kama kazi yao inatambulika; hiyo ninaiwacha kwa yule aliyesema niombe msamaha.

Walimu tulio nao katika maeneo yaliyo na shida tunaomba kupitia hii Hoja watambulike na wapewe marupurupu yao ili wasaidike. Nikiongezea, hakuna anayetaka shida lakini hata sisi waheshimiwa tunachangia watu wetu kupata shida kule mashinani. Boma hujengwa na wenye boma; ukisikia boma fulani walijenga kuko vizuri ni wale waliozaliwa pale ndio wamepafanya hivyo. Tunasikitika na mambo wanayopitia walimu sehemu hizo kame na tuna ndugu zetu walio na uwezo wa kubadilisha hizo hali lakini wanapopata nafasi wanakimbilia mijini. Hapa tumesikia kwamba hata wanashindwa kukodisha mahali pazuri na barabara pia ni mbaya tunangoja kina nani watufanyia haya? Ni sisi tunaotoka katika hayo maeneo tupigania kugeuza hiyo hali.

Nilibahatika kuoa maeneo haya na nataka kusema kwamba nina wake wawili wa kutoka maeneo hayo; mmoja anasema hata nifanywe nini siwezi rudi Bamba na nimefika kwa sababu shida zilizo kule sitaki tena. Ishara yake kubwa ni kwamba watu wanahama kwao na hawataki kukujenga; tusimame tujenge kwetu. Huu ni ugatuzi na umeletwa ujenge kila mahali ambapo palikuwa pamesahaulika ndio maana ya ugatuzi. Nasema asante kwa nafasi hii. Naunga mkono Hoja hii.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Kabla hujamaliza mheshimiwa wacha tumpe Mheshimiwa Grace ana *intervention*.

Hon. (Ms.) Grace: Asante, Bw. Spika. Nimemsikiza mheshimiwa aliyekuwa Sakafuni lakini nimefika mahali nikapotea. Nashangaa tunaongea kuhusu chekechea ama kujenga nyumba ama kuhusu Bamba?

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante, mheshimiwa Grace. Pengine kwa sababu muda wake ulikuwa umeenda naomba akanushe swala ambalo mheshimiwa Grace ameuliza. Je, ni kuhusu kujenga Bamba, barabara ama nyumba ama pia kuhusu mjadala?

Hon. Tete: Nilitaka kutamatisha hapo lakini alivyonipa nafasi nitamueleza aelewe. Tunazungumzia maeneo ambayo yana shida na tunataka walimu wa vyuo vya ufundi vilivyoko ndani ya Kilifi wapigania kuwalipa mapato yao. Shida zingine tunazichangia sijui kwa nini anasema hakuelewa.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Kabla turudishe nafasi hii kwa aliyeleta Hoja wacha tumpe mheshimiwa Rafiki.

Hon. Rafiki: For the benefit of our ECDE teachers to have a friendly working environment and to those who are married to ECDE teachers to have a good environment as suggested by the Leader of Minority, I stand to support. Before I resume my seat, by the mood of the House I suggest that you request the Mover to respond.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Hon. Rafiki, I have given you a chance and you are throwing it to the Mover I will go by that. I have seen a hand from hon. Thaura, what do you have to say?

Hon. Thaura: Asante kwa hii nafasi kuchangia Hoja hii. Nataka kutofautiana na waheshimiwa karibu wote ambao wamechangia. Labda tu nitakubaliana kwa asilimia fulani yale yaliyoongelewa na mheshimiwa Sidi. Mimi siungi mkono asilimia mia hii Hoja kwa sababu ya kile wazungu wanaita “*we are putting the cart before the horse*”. Tuko na maswala mengi ya kuzungumzia, mheshimiwa Spika, kuliko kuzungumzia maswala ya watu kuongezwa mishahara. Alichozungumza mheshimiwa Sidi japo yeye ameunga mkono amezungumzia swala la *wage bill*. Leo tukipitisha kwamba walimu waongezwe mishahara, kesho litakuja kundi lengine pia liombe kuongezwa mishahara, kesho kutwa watatokea wengine pia watake kuongezwa mishahara...

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): There is an intervention from hon. Joseph (Munyoki), so please take your seat hon. Thaura.

Hon. Munyoki: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa fursa hii. Mheshimiwa Thaura nafikiri kuna mahali ananipoteza. Sidhani kama hii Hoja kuna mahali imetaja mishahara. Hii Hoja inaongea kuhusu posho la walimu ambao wako katika sehemu zenye shida, labda anifafanulie.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Mheshimiwa Thaura, labda nikupe muongozo ni kwamba tunajadili kuhusu walimu wa chekechea na wale ambao wako katika vyuo vya ufundi katika sehemu ambazo zina makali ya maisha. Hatuongei kuhusu mishahara.

Hon. Thaura: Mheshimiwa Spika, wacha nikushukuru ila si kwamba nimepotea njia. Tunazungumzia *resource basket* ambayo iko katika Kilifi Kaunti, kwa hivyo kama ni marupurupu ama nyongeza ya namna yeyote bado itatoka katika mfuko ambao tuko nao. Ndio nimezungumza kwamba katika ule mfuko ambao tuko nao tukifikiria sana tunaongeza marupurupu kwa namna ndugu yangu alivyozungumza, basi kila mmoja anapolalamika kwamba aongezwe mwisho wa siku tutaingia katika kuila *recurrent budget* mpaka tuingie kwa *development budget*.

Hata ningeomba waheshimiwa tutokee tupunguze mishahara yetu na marupurupu ili tusaidie katika maeneo ambayo yana matatizo kushinda kuja kusimama kusema watu fulani waongezwe marupurupu.

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza kuna vijana ambao wako nyumbani huko tunakotoka ambao afadhali hao walimu wa ECDE wana mishahara. Kuzungumza kwamba tunaongeza marupurupu ni kwamba tumesahau wale ambao hawana hata kile kidogo. Ni juzi tu

...

Hon. Ziro: Asante sana, mheshimiwa Spika. Ningetaka niongee hili kuhusiana na mheshimiwa ambaye yuko kwa Sakafu ya kwamba huu mjadala ambao uko hapa ya kwamba tuangalie wafanyikazi kuongezwa marupurupu ni kwa sababu niko na imani kwamba mheshimiwa Mwambire alifanya utafiti hata pia kule wewe unakotokea pia zile chanagamoto ambazo wanapitia hao walimu wa chekechea na wale ambao wanafunza hivi vyuo vya ufundi ni changamoto nyingi sana na kufikiria ...

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Mheshimiwa Ziro, ulikuwa ni uulize nafasi kulingana na ...

Hon. Ziro: Mheshimiwa Spika, najaribu kumuelekeza ...

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Mheshimiwa Ziro, hebu kaa chini. Nafikiri sheria za Bunge tunazijua na kama ulikuwa unapitisha ujumbe kwake ilikuwa ni mpaka tumuulize kama yuko tayari kueleza.

Hon. Thaura: Nitamsamehe, ni ndugu yangu na alikuja juzi kwa hiyo anaendelea kujifunza taratibu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka ni juzi tulikuwa na *tournament* ya *Governor's Cup*. Tunavyozungumza kile kitita ambacho kilikuwa kipewe washindi sidhani kama kwao kimefika. Nafikiri hayo ndio maswala ambayo tunastahili kuzungumzia; wale ambao hawajapata fursa si kwa sababu si wahitaji ndugu zangu ambao wanafundisha chekechea ila mimi nazungumzia kwa wale wengi ambao kwa sasa hivi hawajafikiwa na hayo ndio mawazo ambayo waheshimiwa wanastahili kuwa nayo. Kugusa wale ambao hawajafikiwa kufikia sasa hivi.

Tunavyozungumza, wale *support staff* katika *dispensaries* na *health centres* wengi wametamani kuacha kazi kwa sababu hawajalipwa, wacha hapa marupurupu. Hawajalipwa mishahara kwa zaidi ya mwaka mmoja. Hayo ndio mambo ambayo tunastahili kwa sasa hivi tuwe tunazungumzia kwa Bunge hili.

(Hon. Brown stood on a Point of Information)

Hon. Brown: *Mr. Speaker*, naona ndugu yangu anatupotosha. Mimi ni mwalimu na naomba unipatie nafasi hii nimfahamisha jambo moja tu.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Sasa nakuuliza hoja yako ni ya ufahamisho ama?

Hon. Thuara: Sitaki kufahamishwa.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Haya, yeye amekataa kufahamishwa.

(Laughter)

Hon. Brown: Lakini, Bw. Spika, anapotosha.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Kaa chini tafadhali. Mheshimiwa Thaura Mweni, kwa heshima ningetaka tu usimame utuambie tu kama unaunga mkono ama unapinga Hoja hii.

Hon. Thuara: Mheshimiwa Spika, nafikiri kwa heshima ungenipatia muda nikatoa kauli zangu kwanza...

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Umemaliza dakika mbili unusu, jaribu umalize ndani ya dakika mbili.

Hon. Thaura: Asante. Kwa hivyo, ndugu zangu naona wamechemka sana katika kutetea hiyo Hoja ila mimi kama nilivyosema nina mawazo tofauti kabisa kwamba tufikie wale ambao hatujawafikiwa kwanza. Anayeongezwa ashapewa. Napinga Hoja. Asante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Naomba nimpe nafasi hii mheshimiwa Mohamed ili amalizie Hoja hii.

Hon. Mohammed: Thank you, Mr. Speaker. I wish to take this opportunity to thank all Members of this honourable House who have stood and supported this Motion.

I also wish to take this opportunity to clarify the following. That hardship allowance is just an extra amount of money someone is paid for working in different conditions. The conditions that allow for hardship allowances are as follows; areas with rampant insecurity, drought-prone areas, areas lacking essential amenities like hospitals, roads and water and areas with harsh climatic conditions.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The situation in Kilifi County is one among the 17 counties that the TSC has mapped for hardship. In fact, Kilifi is mapped as number three. Members of this House, I would wish *mheshimiwa* Thaura is within the House so that we can inform him. Whatever he has said here is important but we want to urge him that if he sees all that he has said is of much importance to Kilifi people, he drafts a Motion or Statement, brings it to this House so that we can approve it.

I feel that, yes, we had a tournament, and the players have not been given what the government had promised, that is a Statement or a question that he should put in this House through the Chairperson of Sports and Gender Committee to ask the Department of Sports why up to now they have not yet paid the players. But counter-attacking the Motion which is to give relief to our teachers and our VTC trainers is misleading this House.

Again, I would wish to clarify that whatever we want to give, the extra amount that we want to give to our ECDE Teachers and VCT trainers does not or will not be of much difference in such a way that our development amount will be taken to them, no.

Kilifi County gets a bigger share because it is in a hardship area, we are getting a lot of money because of the hardship areas but the rightful people of these areas are not getting that share. How much money has been spent and this House may not be able to ask? So, giving this small amount to our teachers to me is of much importance. I would want to join the Members and request the Members in this House to approve this Motion.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): There is an intervention.

Hon. Mohamed: Is it a Point of information or?

Hon. Ngirani: Mr. Speaker, there is a difference between VCT and VTC.

Hon. Mohamed: Is it a Point of information or?

Hon. Ngirani: A point of clarification Mr. Speaker, VCT and VTC. Vocational Training Centre and Voluntary Counseling ...

(Laughter)

Hon. Mohamed: Thank you, for that clarification hon. Ngirani. But I want to take this opportunity because we have taken a lot of time already debating the Motion to thank all Members more so, hon. Thomas Chengo (Mumba) for amending and adding the vocational trainers to this Motion. I wish this House approves this Motion because most of us here or all the Kilifi County wards are affected by this Motion. We understand there are so many other issues that are of importance to Kilifians.

The Governor has been promising and I believe he will fulfil the promises of employment he has been telling us that soon employment will be advertised for 2,000 youths, women and old people. He has promised us 200 for the Security Department. So, all these are important, and they will be covered if *mheshimiwa* Thaura feels they are taking too long, then he should come up with a Statement or a Question so that the majority side can take it to the Governor for a response as quickly as possible. Otherwise, I thank you Members and I wish to beg the House to approve the Motion. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Thank you, hon. Mohamed Kadhengi for your response.

(Question of the Motion as amended put and agreed to)

ADJOURNMENT

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): So, there being no other agenda on the Order Paper, this House is adjourned until 2:30 p.m.

The House rose at 11:07 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*